Asili ya METHODISTI

Masomo ya Wiki Saba
kwa Vikundi Vidogo

KANISA LA KIMETHODISTI
ULIMWENGUNI

Umethodisti katika ubora wake si chochote zaidi na pungufu bali ni Ukristo hai na thabiti. Kama John Wesley alivyosema, ni dini ya Biblia, dini ya kanisa la awali na dini ya Kanisa la Uingereza. Sisi kama Wamethodisti Ulimwenguni tunataka kukumbatia yaliyo bora zaidi ambayo ni urithi na utamaduni wetu. Lakini hiyo inamaanisha tunahitaji kuukumbuka na kuuelewa.

Katika *Asili ya Methodisti*, mfululizo maalum wa mafundisho na Baraza letu wa Maaskofu, utagundua historia ya Umethodisti na kuelewa jinsi sifa muhimu za imani zinavyoathiri kanisa leo.

Anza kwa kutazama video ya *Asili ya Methodisti*. Video hii ilirekodiwa nchini Uingereza na inaangazia maeneo muhimu ya Wesley yanayotuunganisha na urithi wetu wa Kimethodisti. Baada ya kutazama video, tumia mwongozo huu wa masomo kuzama zaidi katika mada ukiwa na kanisa lako, kikundi kidogo au katika muda wako wa ibada binafsi. Katika mfululizo wote, utajifunza pia kuhusu maeneo muhimu na matakatifu ambayo yanatumika kama ukumbusho wa uaminifu na wito wa Mungu. Kila wiki, utapata kuona sehemu fupi za maeneo haya muhimu—kutoka Chapel ya Wesley jijini London hadi nyumbani kwa Charles Wesley huko Bristol.

Changanua ili kutazama somo la video

Unaweza kutazama video kwa Kiingereza, Kifaransa, Kikorea, Kihispania na Kireno katika globalmethodist.org/methodist-roots.



Somo la 1

KIJINGA KILICHOTOLEWA MOTONI

Mpango wa Mungu wa Kuimarisha Wamethodisti

SOMA

ISAYA 43:1–2

"Lakini sasa, Bwana anasema — Yeye aliyekuumba Yakobo, Yeye aliyekuumba Israeli: 'Usiogope, maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako; wewe u wangu. Unapopita katika maji mengi, nitakuwa pamoja nawe; na katika mito haitakugharikisha. Uendapo katika moto, hautateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza."

WAZA

Mwaka wa 1709, moto uliteketeza nyumba ya familia ya Wesley huko Epworth usiku wa manane. Wakikohoa kutokana na moshi, familia walinusurika moto na kujipata kwenye usiku wa baridi kali. Wote isipokuwa mmoja. Majirani waliona uso wa John uliojaa hofu, aliyekuwa na umri wa miaka mitano, kupitia dirisha la chumba cha juu, huku moto ukiwaka kwa nguvu chini yake. Hakukuwa na muda wa kutumia ngazi. Jirani mmoja alipanda juu ya mabega ya jirani na kumnusuru mvulana kupitia dirisha muda mfupi kabla ya paa kuporomoka kwa kishindo kwa miale ya moto.

John Wesley hakuwahi kusahau tukio hilo. Kwa maisha yake yote, alirudia tena na tena maneno hayo kutoka kwa nabii Zekaria — *kijinga kilichotolewa motoni.* Mungu alimnusuru motoni kwa kusudi. Alikuwa na uhakika kabisa kuhusu hilo.

Imani hiyo ilibadilisha mambo yote maishani mwake. Wakati kundi la Wamethodisti lilianza kukua karibu naye, Wesley aliuliza swali lilo hilo kwa kiwango kikubwa: *"Tunaweza kuamini kuwa mpango wa Mungu ni upi katika kuwakuza wahubiri wanaoitwa 'Wamethodisti'?"* Ni aina ya swali ambalo mtu anayemwamini tu Mungu mwenye kusudi ndiye anayeweza kuuliza. Si, hili lilifanyika vipi? Bali kwa nini Mungu aliruhusu lifanyike?

Jibu lake, lililoandikwa katika maandishi ya mwanzo ya kundi hili, lilikuwa hili: *"Ili kurekebisha taifa, na haswa Kanisa; kueneza utakatifu wa kimaandiko kwenye nchi."* Jibu la Wesley lilikuwa hili — Umethodisti si kitu kingine ila Imani hai ya Kikristo. Imani halisi, kundi halisi la Ukristo, linalowaka moto wa Roho Mtakatifu. Mwenyewe alionya kuwa huenda Umethodisti ukawa *"dhehebu tupu, lenye udini usio na nguvu."* Moto huo ndio ulikuwa tofauti. Walikuwa kijinga kilichotolewa motoni. Waliokolewa ili kusambaza moto wa wokovu wa Roho Mtakatifu duniani kote.

OMBA

Bwana, wewe ni Mungu anayenusuru na Mungu anayetuma. Nakushukuru kwa sababu hukuniacha mpweke, bali ulinita kwa jina na ukaninusuru kutoka motoni. Nisamehe kwa nyakati ambazo nimeishi kwa ajili yangu binafsi badala ya dunia unayoipenda. Njoo, Roho Mtakatifu — pasha moyo wangu kwa moto wa upendo wako. Njoo, Roho Mtakatifu — tupe mshawasha kwa ajili ya dunia uliyokuja kuokoa. Tufanye kuwa watu wanaojua mpango wako kwetu, na wanaosambaza moto wako duniani kote. Amina.

TAFAKARI

1. Umewahi kuhisi kwamba Mungu alikuokoa kwa kusudi fulani? Ulihisi vipi na ulichukua hatua gani?
2. Wesley aliamini kwamba Mungu aliwainua Wamethodisti ili wabadili dunia. Unafikiri Mungu ameliinua kanisa lako kufanya nini?
3. Unaamini kuwa mpango wa Mungu ni upi kwa kanisa la mtaa uliko? Unaona ushahidi gani?
4. Itakuwa na maana gani kwako — binafsi — kuishi kama mtu ambaye amekuzwa kwa kusudi? Unaweza kuchukua hatua gani moja wiki hii?

GUNDUA

Chapeli ya Wesley

LONDON, UINGEREZA

John Wesley alikuwa akikutana na jamii ya Methodisti jijini London na alihitaji mahali pa kukutana. Alinunua kiwanda kilichoharibika cha kutengenezea mizinga nje kidogo ya mji na kukirekebisha. Kiwanda cha kutengenzea mizinga ilikuwa makao yake makuu ya London kutoka 1739 hadi 1778. Kilikuwa kitovu cha mahubiri na shughuli za Kimethodisti, nafasi iliyotoa makazi kwa John na mama yake Susanna na kuwa na zahanati ya kwanza ya bure London.

Chapeli ya Wesley ilijengwa kwa ajili ya ibada ya sakramenti, ikiwa na madhabahu katika sehemu ya nyuma yenye umbo la nusu duara, nyuma ya mimbari. Mimbari ya sasa imeinuliwa, lakini ina urefu wa theluthi mbili tu ya ile ya asili. John Wesley katika jarida lake anaelezea jengo hilo kama “nadhifu kabisa lakini si zuri.” Kwa miaka mingi, kumbukumbu mbalimbali zimeongezwa kuwakumbuka watu muhimu katika Umethodisti wa Uingereza. Mfalme George III alichangia nguzo za mbao kwa ajili ya jukwaa la juu la ndani ya kanisa lakini nguzo hizo zilibadilishwa na kuwekwa marumaru wakati kanisa lilipotimiza miaka mia. Chumba cha chini sasa kinahifadhi Jumba la Makumbusho la Umethodisti.

Kanisa hilo ni kanisa tendaji lenye ibada kadhaa za kila wiki na huduma zingine.



Somo la 2

MUNGU HUTUMIA NANI?

Susanna Wesley, Wahubiri Walei na Mwito wa Mungu

SOMA

YOELI 2:28–29

"Na baada ya hayo, nitamimina Roho yangu kwa watu wote. Na wana wenu, waume na wake watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono. Tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile nitamimina Roho wangu."

WAZA

Samuel Wesley aliketi kwenye dawati, akisoma Agano Jipya la Kigiriki kwa kutumia mwanga hafifu uliopenya kupitia dirisha la maktaba. Akiwa mbali na nyumbani — tena. Akiwa msomi, alijihisi huru zaidi na vitabu vyake kuliko watu wa parokia yake. Alipokuwa mbali, kitu kipya na kisichotarajiwa kiliibuka jioni katika familia yake wakiota moto. Mkewe Susanna alianza kufanya maombi ya jioni nyumbani kwao. Mwanzoni, ni familia pekee iliyohudhuria. Kisha majirani wakaanza kuhudhuria, na baadaye marafiki wa majirani wakaingia. Ghafla, watu walijazana kwenye lango la nyumba na kuchungulia kwenye dirisha, wakijaribu kusikia sauti yake.

Samuel alipopata habari hiyo, alimwandikia barua ya kumwambia akome kufanya hivyo. Wanawake hawakufundisha. Haikuwa desturi. Haikuwa sahihi. Jibu la Susanna lilikuwa tulivu, la uhakika na imara. *"Kama unataka nikome, nitumie amri yako ya moja kwa moja kwa masharti wazi ya kutosha ya kuniepusha mbele ya hukumu ya Yesu Kristo."* Samuel alisikia hekima katika maneno ya Susanna. Hakuwahi kutuma amri hiyo. Kwa hivyo aliendelea.

Miongo kadhaa baadaye, John alikumbana na tukio kama hilo kwa mhubiri mlei aliyeitwa Thomas Maxfield. Maxfield hakuwa ametawazwa. Hakuwa na digrii ya theolojia, au cheo rasmi, wala ruhusa. Alianza tu kuhubiri wakati John alikuwa ameondoka — na matunda ya mahubiri yake yalionekana wazi kwa wote. Wesley alichukua hatua ya kumzuia, maneno ya Susanna ndiyo yaliyomzuia. *"Chunga unachofanya kuhusu kijana huyo, kwa kuwa yeye ameitwa na Mungu kuhubiri kama wewe ulivyoitwa."* John alisikia hekima hiyo hiyo katika maneno ya mama yake ambayo baba yake alijifunza kuamini. Alisikiliza. Kwa hivyo Maxfield aliendelea.

Kutokana na Susanna, John Wesley alijifunza kile ambacho kanisa lilikuwa limesahau — Roho wa Mungu hawezi kuzuiwa na desturi au stakabadhi. Roho anatembea kama mwali wa moto kupitia kijana ambaye hajawekwa wakfu na kupitia mwanamke anayeongoza maombi ya jioni nyumbani kwake. Kile alichoahidi Yoeli kilikuwa cha watu wote katika kila kizazi. Kile ambacho Susanna na Maxfield walithibitisha bado kinathibitishwa leo — katika kila lugha, katika kila kongamano la Kimethodisti Ulimwenguni, kwa kila mtu aliye tayari kunena.

OMBA

Roho Mtakatifu, huzuiliwi na tunachofikiri kinawezekana au kinafaa. Unadhihirisha upendapo na kupitia unayetaka. Tusamehe kwa nyakati ambazo tumenyamazisha sauti yako kwa wengine kwa sababu ilitokea sehemu isiyotarajiwa. Tupe ujasiri wa Susanna — kunena unapotuita, na kuendelea kunena. Tupe hekima ya Samuel na unyenyekevu wa John — kukusikiza hapa kama maneno yako yanatushangaza. Jidhihirishe kwetu sote, watumishi wako, kama ulivyoahidi. Amina.

TAFAKARI

1. Mungu amewahi kuzungumza nawe kupitia mtu usiyetarajia — mtu ambaye huenda ulitaka kumpuuza? Nini kilifanyika?
2. Susanna Wesley alijibu mwito wa Mungu kimya kimya, bila kutaka kutambuliwa au kuomba ruhusa. Mfano wake unakufahamisha nini kuhusu jinsi unavyoitikia mwito wa Mungu maishani mwako?
3. Samuel na John walipata hekima zaidi kwa kumsikiliza Susanna. Ni nani maisha mwako huwa na hekima unayohitaji kusikia? Unamsikiliza?
4. Kuna mtu katika kanisa au jamii yako ambaye vipaji vyake havitambuliwi? Unaweza kufanya nini ili kubadilisha hilo?

GUNDUA

John Wesley's House

LONDON, UINGEREZA

Nyumba ya John Wesley ilijengwa muda mfupi baada ya ujenzi wa Chapeli ya Wesley. Hapo awali, John Wesley alikuwa akiishi Foundery, lakini mnamo mwaka 1779 hapa palikuwa nyumbani kwake. Ghorofa moja ilikuwa kwa ajili ya matumizi yake na ghorofa nyingine zilikuwa kwa ajili ya wahubiri wageni. Chumba cha mbele kilikuwa ofisi yake na kina dawati na baadhi ya maktaba yake. Madirisha yanaangalia magharibi kuelekea Bunhill Fields na kaburi la mama yake. Kitanda alichofia kiliuzwa mnamo miaka ya 1800, lakini kitanda kinachofanana na hicho kipo katika chumba cha kulala sasa. Karibu na chumba cha kulala kuna chumba kidogo cha faragha ambapo alisali mara kwa mara. Nyumba imerejeshwa ili kuakisi mapambo ya karne ya 18.

Changanua msimbo wa QR ili kutembelea John Wesley's House

GUNDUA


HERE

LIES THE BODY OF
MRS SUSANNA WESLEY,
widow of the Rev. Samuel Wesley, M.A.
late Rector of Epworth in Lincolnshire,
who died July 23 1742,
aged 73 years.

She was the youngest daughter of the
Rev. Samuel Annesley D.D. ejected by the Act of
uniformity from the Rectory of St. Giles's
Cripplegate, Aug. 24, 1662.

She was the Mother of nineteen Children
of whom the most eminent were the
Revs. JOHN and CHARLES WESLEY
the former of whom was under God the
Founder of the Societies of the People
called Methodists.

In sure and certain hope to rise
and claim her mansion in the skies,
a Christian here her flesh laid down,
the Cross exchanging for a crown.

Bunhill Fields Burial Ground

LONDON, UINGEREZA

Bunhill Fields (kifupi cha "Bonehill") ilitumika kama makaburi kwa raia wa London ambao hawakuwa washiriki wa Kanisa la Uingereza. Waliitwa Wapinzani kwa sababu waliabudu katika makanisa mengine ya Kikristo, hivyo kutofautiana na Kitabu cha Sala ya Pamoja. Watu waliozikwa hapo ni pamoja na John Bunyan, mwandishi wa Pilgrim's Progress, Daniel Defoe, mwandishi wa Robinson Crusoe na mtunzi wa nyimbo Isaac Watts. Susanna Wesley alizikwa hapo alipofariki mwaka wa 1742. Haya ndiyo makaburi yaliyo karibu zaidi na Kiwanda cha kutengeneza mizinga. Ingawa alikuwa mshiriki wa Kanisa la Uingereza na mke na mama wa makasisi wa Kianglikana, babu na bibi zake wote walikuwa wapinzani.

Changanua msimbo wa QR ili kutembelea Bunhill Fields Burial Ground

Somo la 3

MOYO ULIOHUISHWA KWA NJIA YA AJABU

Uongofu wa John na Charles Wesley

SOMA

WARUMI 5:1

"Basi, kwa vile tumepewa haki kupitia imani, tuna amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."

WAZA

Meli ilitikiswa juu na chini na upande hadi upande katika giza la dhoruba. Mawimbi yaligonga sitaha. Mlingoti ulikereza. Chini, abiria walishikilia chochote kilicho imara, wakipiga kelele za sala ili kunusurika usiku huo. John Wesley alijiegemeza kati ya kuta, akiwa na uhakika kwamba amekaribia kufa.

Kisha, katika nafasi tulivu katikati ya kelele za mawimbi, alisikia kitu asichokitarajia. Watu wanaoimba.

Kikundi cha Wakristo Wamoravia waliimba nyimbo za sifa, sauti zao zikiwa wazi na thabiti chini ya upepo mkali — watulivu, wamejaa furaha, hawakuogopa kufa. Wesley alitapatapa gizani ili kuwapata. Alisikia amani yao. Yeye alihisi tu hofu.

Tukio hilo lilifunua jambo ambalo miaka ya nidhamu ya dini haikuwahi kufumbua. Alikuwa ametimiza kila sheria. Alikuwa ameomba, kufunga, amelisha wajane na mayatima, na kuwatembelea wafungwa. Na bado aliogopa kufariki. Sheria. Nidhamu. Miaka ya kuweka juhudi. Hakuna hata moja kati ya hayo yalinunua alichohitaji zaidi — maarifa kwamba Kristo alikufa kwa ajili yake na kujitoa kwa ajili yake. Kwamba dhambi zake zilisamehewa kweli.

Nduguye Charles aliipokea kwanza. Mnamo tarehe 21 Mei 1738, Charles hatimaye aliacha kujitahidi na akamwamini Kristo pekee kwa wokovu wake — na msamaha alioutafuta ulimjia kama wimbi. Hiki ndicho Wesley baadaye alitaja kuwa imani iletayo haki. Furaha yake ilimiminika kutoka kwa Charles kama tenzi. John alisikia kuhusu amani ya ndugu yake lakini alihisi hofu tu. Aliendelea kutafuta. Aliendelea kuomba. Siku tatu baadaye, tarehe 24 Mei 1738, John aliketi katika nyumba moja Barabara ya Aldersgate wakati mtu alikuwa akisoma kwa sauti kutoka kwenye dibaji ya Luther kuhusu Warumi. "*Takribani robo saa kabla ya saa tatu...nilihisi moyo wangu umehuishwa kwa njia ya ajabu. Nilihisi kwamba namwamini Kristo, Kristo pekee kwa wokovu, na nikapata hakikisho kwamba alibeba dhambi zangu.*"

Nilimwamini Kristo pekee. Hiyo ndiyo imani iletayo haki — imani isiyotokana na juhudi bali inayopokelewa, msamaha wa kutojitafutia bali tunaopewa. Alikuwa ameiona katika amani iliyowaongoza Wamoravia kwenye dhoruba. Aliisikia kwenye furaha iliyomiminika kutoka kwa Charles kama tenzi. Sasa, hatimaye, aliipata. Wesley alitaja tukio hili kama uthibitishaji wake na kuzaliwa upya — mpito wa kukaribia kuwa Mkristo hadi kuwa Mkristo kabisa, kutoka kwa mfano wa imani hadi kwa moto wake. Wesley alitumia miaka hamsini iliyofuata kupeleka zawadi hiyo kwa kila aliyetaka kuipokea. Hii ndiyo Methodisti, kwa ubora wake, imekuwa ikisambaza duniani kila wakati.

OMBA

Bwana Yesu, hukufa ili kunipa dini. Ulikufa ili kunisamehe na kunipa amani na Mungu. Kama John Wesley, nimefuata sheria, nikaomba na kutenda kazi. Na kama John Wesley, wakati mwingine bado ninaogopa. Nimesikia jinsi ilivyo imani iletayo haki. Nimeona inavyofanana kwa wengine. Sasa ninaitaka kwangu. Ninaacha kujitahidi. Ninakuamini — Kristo pekee — kwa wokovu wangu. Ondoa dhambi zangu. Hata zangu. Huisha moyo wangu, Roho Mtakatifu. Nijulishe, kwenye mifupa yangu, kwamba mimi ni wako. Amina.

TAFAKARI

1. Umewahi kukumbana na hali ambapo kile ulichoamini akilini kimekuwa uhalisia uliojua moyoni mwako? Nini kilifanyika?
2. John Wesley alifuata kila sheria ya kidini na bado alihisi kuwa mbali na Mungu. Ushawahi kuhisi hivyo? Nini kilikosekana?
3. Wamoravia walihisi amani katikati ya dhoruba. Amani ya aina hiyo huonekana vipi katika maisha ya mtu? Umeiona kwa wengine? Umeipata mwenyewe?
4. Warumi 5:1 inasema tuna amani na Mungu kupitia imani iletayo haki. Unafahamu amani hiyo? Kama sivyo, itakuwa na maana gani kwako kumwamini Kristo pekee kwa ajili ya wokovu wako?

GUNDUA



Charles Wesley's House

BRISTOL, UINGEREZA

Tofauti na kaka yake mkubwa, Charles Wesley alikuwa na ndoa yenye furaha. Sarah Gwynne alitoka kaskazini mwa Wales na aliamini sana katika harakati za Kimethodisti. Walifunga ndoa mnamo mwaka 1749 na kuhamia Charles Street huko Bristol. Charles alikuwa mhubiri msafiri kama kaka yake na alishiriki katika uongozi wa Unganisho. Hata hivyo, maisha yake ya nyumbani yenye furaha na wito wake kama mtunzi wa nyimbo za dini vilimfanya abaki nyumbani zaidi kuliko John. Katika maisha yake aliandika zaidi ya nyimbo za dini 8,900. Yeye na kaka yake walichapisha vitabu vingi tofauti vya nyimbo za dini. Charles na Sarah waliishi katika nyumba hii ya Bristol kwa miaka 22 na walikuwa na watoto wanane, watatu tu kati yao walinusurika utotoni. Vijana wao Charles na Samuel walikuja kuwa wanamuziki mashuhuri wa kanisa.

Changanua msimbo wa QR ili kutembelea Charles Wesley's House

Somo la 4

MUNGU HUFANYA NINI KATIKA MAISHA YA IMANI?

Utakatifu wa Kimaandiko

SOMA

EZEKIELI 36:26–27

"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu; nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo mwepesi. Nami nitatia Roho yangu ndani yenu, na kuwaongoza katika kanuni zangu, nanyi mtazifuata sheria zangu."

WAZA

John Wesley alikuwa akiandika shajara. Si aina ile ambayo mtu huandika matukio ya siku yake, bali ile ambayo mtu hujipima na Mungu. Kila saa inawajibikiwa. Kila tukio la kushindwa linaandikwa. Aliwatembelea wafungwa kwenye magereza yao baridi. Alianzisha shule kwa watoto ambao hawakuwa na chochote. Alifunga hadi akawa mdhaifu. Aliomba hadi magoti yakawa na maumivu. Na kila mwisho wa siku, alifungua shajara yake na kujiuliza swali lilelile gumu — imetosha?

Haikutosha hata kidogo.

Huu ndio mtego ambao utakatifu huwa tunapouelewa vibaya. Shindano la kujipima ambalo hatuwezi kushinda. Kiwango tunachokaribia kufikia lakini hatufikii. Wesley alifahamu mtego huu kwa undani. Aliujenga kwa mikono yake mwenyewe. Hivi ndivyo alivyokuwa kabla ya Aldersgate.

Lakini Mungu aliyenena kupitia Ezekieli alikuwa na dhana tofauti kabisa. Si kiwango cha juu cha kufikia, bali kupokea upandikizaji wa moyo. Nitaondoa moyo wa jiwe, nitawapa moyo mwepesi. Mtu anayekimbia ghadhabu, akijipima dhidi ya Mungu katika kurasa za shajara, hawezi kupata moyo mpya kwa kujitahidi. Mungu alilazimika kutoa. Katika Aldersgate, Wesley aliupokea. Hofu ikaondoka. Imani na msamaha vikaja. Na Roho aliyeingia alianza kumbadilisha kuanzia ndani kuelekea nje. Sasa kazi yake ilifanyika si kwa jitihada, bali kwenye hazina ya kina ya amani, upendo, na shukrani.

Hii ndiyo Wesley alitaja kuwa utakatifu wa kimaandiko. Si utakatifu wa shajara na kipimo, bali utakatifu wa moyo uliobadilishwa. Hakuna shajara ingeweza kuzalisha haya. Hamna nidhamu ingeweza kuipata. Neema pekee huumba haya.

Mabadiliko haya si kitu tunachopata kwa bidii. Ni kitu tunachopokea. Maandiko yanafafanua matunda yake matakatifu kwa urahisi — upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi. Si orodha ya sheria za kufuata, bali ni mbubujiko asili wa maisha ambayo Roho anaishi ndani yake. Moyo mwepesi, sio wa jiwe — ukipiga zaidi kama moyo wa Mungu.

Utakatifu wa kimaandiko haukupaswa kuwa mafanikio ya wachache pekee. Ni haki ya kuzaliwa ya kila mtoto wa Mungu.

OMBA

Bwana, mara nyingi nimejaribu kutafuta kile ambacho umenipa kila wakati bila malipo. Ondoa jiwe moyoni mwangu. Nipe moyo mwepesi. Nijaze kwa Roho wako. Nifanye kuwa mtu ambaye upendo, furaha na uvumilivu wake si matokeo ya juhudi zangu mwenyewe, bali ni mbubujiko w maisha yako ndani yangu. Haya ndiyo mapenzi yako kwangu. Nayapokea. Amina.

TAFAKARI

1. Umeshawahi kuhisi imani kama shindano la kujipima ambalo huwezi kushinda? Ulihisi vipi?
2. Maandiko yanafafanua tunda takatifu la maisha yaliyobadilishwa na Roho kama upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, wema, uaminifu, upole na kiasi. Unatamani lipi kati ya haya likuzwe na Mungu ndani yako?
3. Inamaanisha nini kumwamini Roho ili azalishe matunda mengi matakatifu na tele katika maisha yako?
4. Wesley aliamini Roho anaweza kubadili moyo wa mwanadamu kiasi kwamba upendo — si wajibu, si hofu, si hatia — uwe motisha ya kweli na ya kina zaidi. Unaamini kwamba hilo linawezekana? Unaitaka mwenyewe?

GUNDUA



Pill Sailing Site

PILL, UINGEREZA

Katika miaka ya 1700, Bristol lilikuwa jiji la pili kwa kukubwa nchini Uingereza na bandari kuu kwa wale waliosafiri kwenda Amerika. Meli zilitia nanga kwenye maji marefu na abiria walichukua boti ndogo kutoka ufukweni hadi kwenye meli. Moja ya sehemu hizo za kuanzia safari ilikuwa kijiji karibu na Bristol kiitwacho Pill. Kutoka eneo hili, Thomas Coke, Richard Whatcoat na Thomas Vasey walianza safari kutoka Pill kwenda Amerika mnamo Septemba 18, 1784. Siku chache kabla, John Wesley alikuwa amewatawaza Whatcoat na Vasey kama mashemasi na wazee, na kumfanya Coke kama mrakibu mkuu wa kazi huko Amerika. Katika Mkutano wa Krismasi huko Baltimore, wahubiri wa Kimarekani waliwachagua Coke na Asbury kuwa maaskofu. Katika siku zilizofuatana, Coke alimweka Asbury wakfu kuwa shemasi na kisha mzee, halafu akamweka wakfu kuwa askofu.





Somo la 5

KWENDA NYANJANI

Ari ya Uinjilisti

SOMA

LUKA 4:18–19

"Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiria maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwapa uhuru wanaoteswa, kutangaza mwaka wa neema ya Bwana."

WAZA

Hawakuwa watu waliokwenda kanisani. Walikuwa wachimbaji wa makaa — wanaume walioteremka katika migodi hatari kabla ya kucha na kutoka tena jioni, nyuso zikiwa nyeusi na wakiwa wamechoka sana. Viti vya kanisa vilikuwa vya waheshimiwa, lugha ya kanisa ya wasomi. Milango ya kanisa ilikuwa wazi kinadharia lakini imefungwa kimatendo kwa yeyote aliyefunikwa mavumbi ya makaa na harufu ya jasho kutokana na kazi ngumu.

Mnamo Februari 1739, George Whitefield alitembea nyanjani nje ya Bristol na akaanza kuhubiri. Alijifunza ukweli wa ajabu kwamba ingawa kanisa halingeenda kwa wachimbaji, wachimbaji walikuja kwa mhubiri. Umati ulikusanyika ambao hata kanisa halingeweza kumudu wala kutaka kumudu. Alimwandikia rafiki yake John Wesley akamhimiza ajiunge naye.

Wesley alisita. Alikuwa mhudumu wa Kanisa la Uingereza. Watu waliotawazwa walihubiri kutoka mimbari ya kifahari, ni kwenye nyanja zenye matope. Kuhubiri nje hakukufaa na kulisababisha aibu. Kila kitu katika hali yake ya ustaarabu kilipinga hilo. Ilikuwa na kasoro. Lakini ilikuwa makosa? Mnamo tarehe 2 Aprili 1739, aliandika kwa unyenyekevu kwenye jarida lake kwamba alikubali *"kujidunisha zaidi"* na akaenda nyanjani. Maandiko aliyochagua yalibaini alichoamini — kuwa Mungu alikuwa na habari njema kwa maskini.

Alichokiona Wesley akiwa juu ya kisiki cha mti kwenye uwanja huo kilimbadilisha daima. Watu elfu tatu au nne, wenye njaa ya injili, wamesimama katika uwanja. Watu ambao kanisa lilikuwa limewapuuzilia mbali. Wesley alitazama na kuona haswa wale Yesu alioita — maskini, mateka, vipofu, walioonewa. Alifahamu lengo lake.

Imani ambayo Wesley alipokea katika Aldersgate, na tunda takatifu ambalo Roho alikuza moyoni mwake, halikupaswa kuwa lake pekee. Siku zote tunda lilipaswa kutolewa kwa wengine. Uwanja ule nje ya Bristol ndipo ukarimu ulianzia. Kutokana na uwanja huo, Wamethodisti walipata ari takatifu iliyokataa kusubiri hadi waumini waje kanisani. Hii ndiyo ilikuwa misheni yao — kupeleka nuru ya injili kwa watu wanaoishi gizani. Walikwenda kwenye barabara za miji yenye umati mkubwa wa watu, migodi yenye giza na nyanja zenye matope — popote ambapo watu walikuwa maskini wa roho na wenye njaa ya neema. Walitumwa kupeleka moto wa wokovu wa Roho Mtakatifu kwa kila pembe ya dunia.

OMBA

Bwana, nisamehe kwa nyakati ambazo nimesubiri kwa starehe waliopotea ili wakuje kwako wenyewe. Nipe ari ya Wesley katika uwanja huo — utayari wa kuchagua kutokuwa na starehe, kuonekana mjinga, kwenda mahali ambapo tayari unafanya kazi. Nipake mafuta na Roho wako ili nipeleke habari njema kwa maskini, uhuru kwa mateka, nuru kwa watu wanaoishi gizani. Na unipe ujasiri wa kuchukua hatua. Amina.

TAFAKARI

1. Ni watu wapi katika jamii uliko hawawezi kuthubutu kuingia katika kanisa uliko? Nini kinawafanya wasiende?
2. Wesley "alikubali kujidunisha zaidi" — ikimaanisha alikuwa tayari kuonekana duni kwa ajili ya injili. Utayari kama huo utakugharimu nini?
3. Yesu alisema amepakwa mafuta kuleta habari njema kwa maskini, uhuru kwa mateka, na kuona kwa vipofu. Maskini, mateka na vipofu ni akina nani katika jamii yako?
4. Ni hatua gani moja ambayo kanisa lako linaweza kuchukua ili kuwafikishia watu injili ambao hawatawahi kuitafuta wenyewe?



GUNDUA



John Wesley's New Room

BRISTOL, UINGEREZA

Pamoja na Wamoravia na wengine, John Wesley alianzisha jamii za kidini kusaidia watu kupata wokovu. Kulikuwa na jamii mbili huko Bristol, lakini baada ya kuanza kuhubiri nje, watu wengi zaidi walijiunga na jamii hizo. Ili kutoa nafasi kwa vikundi vilivyokuwa vikikua, Wesley alipata ardhi katika wilaya ya Bristol iitwayo Horsefair na akajenga jengo. Ni sehemu ya ibada ya Kimethodisti ya zamani zaidi duniani, iliyoanzia mwaka wa 1739. Ilitumika kwa ibada za mahubiri, mikutano ya wengi, zahanati na huduma kwa maskini. Kuanzia mwaka wa 1744, wahubiri wa Kimethodisti katika unganisho na John Wesley walikutana kwa mkutano kila mwaka, na baadhi ya mikutano hiyo ilifanyika katika Chumba Kipya.



Somo la 6

TUNAWEZA KUIMARIKA VIPI PAMOJA KATIKA UTAKATIFU?

Uwajibikaji na Mikutano ya Wengi

SOMA

YAKOBO 5:16

"Ungameni dhambi zenu kati yenu na kuombeana ili muweze kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu na husikika."

WAZA

Ilianza kwa deni. Wesley alikuwa amekopa fedha ili kujenga Chumba Kipya huko Bristol — nyumba ya kuhubiri kwa jamii ya Methodisti inayokua — na mkopo wa nyumba ulipaswa kulipwa punde. Mtu alipendekeza washirika wagawanywe kwa makundi ya watu kumi na wawili. Kila mmoja alipaswa kulipa senti moja kwa wiki. Kiongozi angetembelea kila mshirika nyumbani kwake, achukue senti,, aweke akaunti, na kuhakikisha kuwa kila mtu alichangia. Rahisi. Halisi. Isiyo ya kiroho kabisa.

Lakini kitu kisichotarajiwa kilifanyika.

Viongozi walipoanza kuwatembelea walioko chini ya uangalizi wao, waligundua kuna washirika ambao hawakuwa wakiishi inavyostahili. Baadhi yao hawakuwa wakiishi kwa amani na majirani zao. Wengine walirejelea desturi na mienendo ya dhambi katika maisha.

Walipopeleka ripoti kwa Wesley, ni kama swichi iliwashwa. Ghafla akatambua kile ambacho jamii za Methodisti zilikuwa zimekosa muda wote — mfumo wa uwajibikaji wa kiroho.

Kilichoanza kama mbinu halisi ya kukusanya ada za ushirika kikawa kitu muhimu zaidi. Ikawa njia ya kutunzana kwa upendo.

Wesley akaweka desturi hiyo kuwa rasmi. Washirika walipangwa kwa vikundi vidogo madarasa, wakikutana kila wiki nyumbani kwa mtu. Kila kusanyiko lilijumuisha mazungumzo, maombi, mahimizo na tafakari ya kweli. Na kila wiki kiongozi wa darasa aliuliza kila mshirika swali rahisi lakini la kujichunguza — *"Hali ya roho yako iko vipi?"*

Swali hili lilihitaji kitu ambacho kanisa liliacha kuuliza kwa muda mrefu — ukweli. Si ukweli wa kuigizwa Jumapili asubuhi, wakati kila mtu anaingia kanisani akiwa amevaa mavazi mazuri na kuonyesha uso mzuri. Swali hili lilihitaji ukweli wa saa nne usiku, Ijumaa. Swali hilo halikuwaruhusu watu kujificha. Mwanaume alikiri kwamba hakuwa na ushirika na Mungu wiki nzima na hakusoma Biblia yake. Kijana alikiri kwamba alimzungumzia baba yake kwa dharau. Mwanamke alikiri kwamba alikuwa na uchungu dhidi ya jirani. Na katika kukiri huko, kitu fulani kilianza kubadilika. Hivi ndivyo utakatifu ulivyotokea — si kwa upweke, bali pamoja, katika jumuiya ya kweli ya watu walioouliza swali gumu zaidi.

Wesley alielewa kwamba kwa upana tumesahau — kuwa utakatifu si juhudi ya mtu mmoja. Moyo uliobadilishwa haufanyi kazi kwa kujitenga. Unahitaji joto la jamii ya kweli, ushirika wa sala pamoja na uwajibikaji wa watu wanaojua jina na aibu yako na hawatakuruhusu upotee. Hatuwezi kuwa watakatifu tukiwa peke yetu. Hatukuwahi kuwa. Hatutawahi kuwa.

OMBA

Bwana, tunakiri kwamba mara nyingi tumejaribu kukufuata kisiri na peke yetu, tukificha mambo tunayong'ang'ana nayo kwa wale wanaoweza kutusaidia kuyabeba. Tusamehe kwa kuigiza imani bila kuitenda. Tujalie ujasiri wa kuuliza na kujibu swali gumu — hali ya roho zetu iko vipi? Tuunganishe pamoja katika jamii ya kweli. Tufanye watu tunaoambiana ukweli kwa upendo, kuombeana kwa imani, na kukataa kutengana. Amina.

TAFAKARI

1. Kuna mtu yeyote maishani mwako anayejua jibu la kweli kwa swali — hali ya roho yako ni ipi? Kama hakuna, ni nini kimekuzuia kuingia kwa mahusiano kama hayo?
2. Ni nini huwazuia watu — ni nini hukuzuia — kutumia aina ya ukweli ambao unahitajika katika mikutano ya wengi? Ni nini kingehitaji kubadilika ili kanisa lenu kuwa aina hiyo ya jamii?
3. Wesley aliamini kwamba wakati roho ya mtu inamkaribia Mungu, maisha yake yote hubadilika. Umeona hilo likifanyika — katika maisha yako au ya mwingine?
4. Itakuwaje iwapo kanisa lako litarejelea desturi hii? Unaweza kuchukua hatua gani wiki hii itakayosababisha uwajibikaji wa kina zaidi?

GUNDUA

Christ Church College

OXFORD, UINGEREZA

John Wesley alielekea Oxford kutoka Shule ya Charterhouse huko London. Chuo chake kilikuwa Christ Church, labda ndicho chenye hadhi zaidi kati ya vyuo vilivyounda Chuo Kikuu. Alifuzu mnamo mwaka 1725 na kuanza kusomea mitihani yake ya kuwekwa wakfu. Mwaka huo, alisoma kitabu cha Askofu Jeremy Taylor Kanuni na Mazoezi ya Kuishi Kitakatifu na Kufa Kitakatifu. Aligundua kuwa ilikuwa muhimu sana kupima jinsi alivyotumia muda wake. Alianza kuweka shajara ili kupima maendeleo yake kuelekea utakatifu. Mwaka uliofuata alichaguliwa kuwa Mwanazuoni wa Chuo cha Lincoln.



Changanua msimbo wa QR ili kutembelea Christ Church





Somo la 7

MUNGU HUTUSITIRI VIPI?

Mbinu za Neema

SOMA

MATENDO 2:42

"Walijitolea katika mafundisho ya mitume, ushirika, kuumega mkate na kusali."



WAZA

Aliangalia kwa hamu mkate na divai ambayo kuhani alitoa. Lakini hakuondoka kwa kiti chake. Hakuwa na uhakika kuwa ameokoka. Hakuwa na uhakika kuwa anaamini vya kutosha, au kuhisi vya kutosha, au mwenyewe anatosha. Walimu Wamoravia walimwambia wazi — usije mezani hadi uwe na uhakika. Subiri. Kuwa na uhakika kwanza. Kisha upokee.

John Wesley hakukubaliana na hilo. Kabisa.

Si naye. Kwa ushauri aliopewa. Wesley alitumia miaka mingi akifanya matendo kama yake — akisubiri kuwa na uhakika kabla ya kumwendea Mungu. Alifahamu mwisho wa hilo. Alifanya hivyo mwenyewe, hadi kwenye meli katikati ya dhoruba, akiwa na hofu na peke yake. Wamoravia walikuwa sahihi kuamini kwamba hakikisho ni muhimu. Lakini utaratibu wao ulikuwa umegeuzwa kabisa.

Husubiri neema kisha upate ushirika na Mungu kupitia Meza ya Bwana. Unashiriki Meza ya Bwana kwa sababu unahitaji neema ya ushirika na Mungu.

Wesley alitetea kwamba Mungu ameweka njia za kawaida ambazo kupitia kwazo anamimina neema yake kwa watu wanaomtafuta. Aliziita mbinu za neema. Kusoma maandiko. Maombi. Uabudu. Kufunga. Meza ya Bwana. Mazungumzo ya kweli kati ya waumini kuhusu mambo ya Mungu — kile ambacho Wesley aliita makongamano ya Kikristo. Mbinu hizi za neema hazikuwa zawadi kwa walio watakatifu tayari. Zilikuwa njia kuelekea utakatifu. Njia ambayo Mungu hutumia kutembea nasi, akitubadilisha tufanane naye zaidi na zaidi.

Haya ndiyo mambo ambayo Wakristo wa kwanza walielewa bila kufunzwa. Walijitolea kabisa — si mara kwa mara, si wakati walihisi kufanya hivyo, si baada ya kuwa na uhakika wa kutosha — kwa mafundisho, ushirika, kumega mkate, na sala. Walijitolea kwa ushirika, pamoja. Walitumia mbinu za neema kwa sababu walihitaji neema hiyo. Na neema ilikuja kwa sababu walitumia mbinu hizo.

Wesley aliita hii mfumo wa neema — njia nzima ya maisha inayoongozwa na njia ambazo Mungu hutumia kufanya kazi. Huu ndio Ukristo hai ambao Roho humimina kwa watu wote — maskini, waliovunjika, na waliopotea. Tumia mbinu za Mungu. Amini neema ya Mungu. *Mfumo huu wa neema* unachochea moto wa utakatifu wa kimaandiko ambao Wamethodisti Ulimwenguni wanataka kuusambaza kote duniani.

OMBA

Bwana, nisamehe kwa nyakati ambazo nimekaa mbali na wewe kwa sababu sikuhisi kwamba ninastahili kukukaribia. Nisamehe kwa kufikiri kwamba ningeweza kuwa mtakatifu bila kukukaribia. Umenipa mbinu zote za neema ninazohitaji ili kukujua — Neno lako, meza yako, watu wako, Roho wako. Naja sasa, si kwa sababu ni msafi vya kutosha, bali kwa sababu nataka kukujua na kufanana nawe. Kutana nami hapa. Mimina neema yako maishani mwangu kupitia kila njia uliyofungua. Mimi ni wako. Amina.

TAFAKARI

1. Umewahi kukaa mbali na Mungu — na sala, uabudu au meza — kwa sababu hukuhisi unastahili au hukuwa na uhakika wa kutosha? Nini kilikuzuia?
2. Wesley alisema sala, maandiko, uabudu na ushirika ni njia kuelekea utakatifu — si zawadi kwa kuwa mtakatifu tayari. Hilo linabadili vipi unavyofikiri kuhusu desturi hizi?
3. Matendo 2:42 inaeleza kanisa la kwanza kujitolea kwa mambo manne — mafundisho, ushirika, kumega mkate na sala. Lipi kati ya haya ni imara zaidi maishani mwako? Lipi linahitaji umakini zaidi?
4. Itakuwaje iwapo kanisa lako litakuwa jamii inayotembea pamoja kwenye njia ya neema, daima na kwa matarajio?

GUNDUA



Hanham Mount

BRISTOL, UINGEREZA

John Wesley alihubiri nje kwa mara ya kwanza mnamo Aprili 2, 1739. Alisema kwamba kabla ya hapo alikuwa "ameshikilia sana kila jambo linalohusu adabu na utaratibu kiasi kwamba [ange]ona kuokoa roho kuwa kama dhambi kama kusingefanywa kanisani." Alipomwona George Whitefield na kuona umati mkubwa, alitambua kwamba kuhubiri nje kulikuwa njia ya kuwafikia watu. Hanham Mount ikawa mojawapo ya maeneo yake ya kawaida ya kuhubiri nje. Kwa maisha yake yote yaliyosalia Wesley alisisitiza kuwa kupeleka injili mahali ambapo watu walikusanyika nje ilikuwa sehemu muhimu ya huduma ya Kimethodisti.

Asili ya METHODISTI

Asante kwa kusafiri nasi kupitia Asili ya Methodisti, tukitafakari juu ya msingi wa Umethodisti na jinsi tunavyoweza kutimiza wito wa kueneza utakatifu wa kimaandiko kote ulimwenguni.

Unapotafakari juu ya historia yetu tajiri ya Kimethodisti, tafuta njia za kuiishi imani katika maisha yako mwenyewe–iwe ni kuanzisha mikutano ya wengi kama Wesley alivyofanya au kuishi maisha ya Kikristo kwa ukamilifu.





KANISA LA KIMETHODISTI
ULIMWENGUNI

Somo la video la Asili ya Methodisti lilitayarishwa na Kanisa la Methodisti Ulimwenguni kwa ushirikiano na Maaskofu Kimba Evariste, Leah Gregory, Scott Jones, Eduard Kheguy na Mark Webb. Mtaala wa mwongozo wa masomo uliandikwa na Bethany Ross.

Picha zilizopo katika mwongozo huu wa masomo zinaonyesha safari ya Mkutano wa Maaskofu kwenda kwenye maeneo ya kihistoria ya Wesley na Wamethodisti nchini Uingereza. Maeneo muhimu ni pamoja na Chumba Kipya cha John Wesley, Nyumba ya Charles Wesley huko Bristol, Nyumba ya John Wesley jijini London, Christ Church katika Chuo Kikuu cha Oxford, na maeneo mengine.

Kwa maelezo zaidi na kuona mifululizo mingine ya mafundisho, tembelea globalmethodist.org.